

Salamu kutoka Mary Todd Elementary,

Hati hii itakusaidia kumwandaa mtoto wako kufanya mtihani wa MAP Growth. Tafadhali kuwepo nyakati zifuatazo ili kumhimiza mtoto wako anapoufanya mtihani:




**\* Habari juu ya siku na wakati maalum wa mwanafunzi wako zitatoka kwa mwalimu wao \***

## MAP Growth ni nini?



MAP Growth huwasaidia walimu kuelewa kile ambacho wanafunzi wanajua leo, ili malengo yawekwe kuimarisha ukuaji mwaka mzima. **Wanafunzi hawawezi kupita wala kuanguka mtihani huu.**



**Mtihani huu hautaathiri alama.** Kwanza, ni kawaida kwa wanafunzi kujibu tu nusu ya maswali kwa usahihi. **Tafadhali usiwasaidie!**



Kutokana na changamoto za masomo kutoka nyumbani, matokeo ya mtihani wa MAP Growth ni muhimu sana kwetu mwaka huu. **Matokeo haya yatatusaidia kujua kile ambacho wanafunzi wako tayari kujifunza.**

## Maandalizi ya Mtihani

### Kabla ya Siku ya Mtihani

1. Hakikisha kuwa kifaa chako kina muunganisho wa mtandao
2. Lemaza uzuiaji wa ibukizi kwenye kivinjari chako cha wavuti
3. Hakikisha kuwa kifaa chako kinatimiza matakwa ya mtihani kwa kutumia [Workstation Diagnostic Tool](#)
4. Hakikisha kuwa mtoto wako ana visikizi vya masikioni
5. Tazama video ya utangulizi [wa MAP Growth](#)
6. Jaribu mtihani kwenye [practice.mapnwea.org](#) (Jina la Mtumiaji: grow, Nywila: grow)

### Siku ya Mtihani

1. Punguza usumbufu kwa mtoto iwezekanavyo
2. Hakikisha kuwa mazingira ya mtihani ni matulivu
3. Mruhusu mwalimu/mlezi wa mwanafunzi afungue kipindi kwanza
4. Ingia kwenye [test.mapnwea.org](#)
5. Hakikisha kuwa una njia ya kuwasiliana na mwalimu/mlezi wa mwanafunzi wakati wa mtihani
6. Fuata maagizo yoyote ya ziada kutoka kwa mwalimu/mlezi wa mwanafunzi

